



## HIFADHI ZA TAIFA TANZANIA

### TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

*Kilimanjaro, Oktoba 12, 2020*

#### JITIHADA ZINAENDELEA KUDHIBITI MOTO MLIMA KILIMANJARO KATIKA ENEO LA WHONA – HOROMBO

Moto uliozuka jana Mlima Kilimanjaro katika eneo la Whona, ambacho ni kituo cha kupumzikia wageni wanaotumia njia ya Mandara na Horombo unaendelea kudhibitiwa na vikosi vinavyoshiriki zoezi hilo. Vikosi vinavyoshiriki vinajumuisha wananchi, wanafunzi wa mafunzo kwa vitendo na wale wa Chuo cha Mweka na Kikosi cha Zimamoto

Taarifa zaidi kuhusu chanzo zinaendelea kufanyiwa kazi.

TANAPA inaendelea kuchukua tahadhari zote ili kuhakikisha kuwa usalama wa wageni na vifaa vyao unaimarika bila kuathiri shughuli za utalii ambazo zinaendelea kama kawaida hususani kwa njia ya Marangu iliyoathirika na moto husika.

Imetolewa,

Pascal Shelutete

Kamishna Msaidizi Mwandamizi – Mawasiliano

**TANAPA**